



CHAGUA CCM



SAIDI ALLY MSOMOKA
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA TANDAHIMBA

HALMASHAURI

ya wilaya ya Tandahimba ilivyotumia mabilioni kutatua changamoto za wananchi kila kona





CHAGUA CCM

Mikopo yamwagwa kwa vijana, wanawake, watu wenye ulemavu



MUONEKANA wa madarasa mapya Shule ya Msingi Lipalwe

Na MWANDISHI MAALUMU

WAKATI zao la korosho likiwa katika nafasi ya juu katika kutoa mchango wake kwa maendeleo ya uchumi wa taifa hususan kupitia kilimo, Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba ndiyo wilaya inayoongoza kwa uzalishaji wa korosho nchini.

Hatua hiyo imefanya wilaya hiyo katika kipindi cha miaka mitano tangu kuingia madarakani kwa serikali ya awamu ya tano chini ya Rais Dk. John Magufuli, kupiga hatua kubwa ya maendeleo.

Katika kipindi hicho cha miaka mitano, Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba inajivunia kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo iliyoleta tija kwa wananchi kwa kuwaondolea adha mbalimbali na kuongeza tija katika maisha ya kila siku.

Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Saidi Msomoka, akizungumzia miaka mitano ya serikali ya awamu ya tano chini ya Rais Dk. Magufuli kwa halmashauri yake, anasema imekuwa na maana kubwa kwa uchumi na sekta zote katika kufanikisha ustawi wa jamii.

Msomoka anasema katika kipindi hicho, Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba imefanikiwa kutekeleza miradi yenye thamani ya sh. bilioni 11.698, katika sekta mbalimbali za maendeleo.

Takriban aslimia 85 ya fedha zote zinazopatikana katika Halmashauri ya Wilaya Tandahimba chanzo chake ni zao la korosho.

UJENZI WA VITUO VYA AFYA ULIVYOWAKOMBOA WANANCHI

Sekta ya afya ikiwa ni moja ya maeneo muhimu kwa maendeleo ya jamii, katika kipindi cha miaka mitano serikali imeitazama kwa jicho la karibu na kufanikisha miradi mbalimbali.

Mkurugenzi anasema moja ya miradi iliyotekelezwa ni ujenzi wa ukarabati wa miundombinu katika Kituo cha Afya Mahuta, ambapo Halmashauri ya Wilaya Tandahimba ilipokea sh. milioni 400, kutoka serikali kuu, kwa ajili ya ujenzi wa ukarabati wa miundombinu ya kituo hicho.

Mchanganuo wake ni kwamba,

ukarabati mkubwa wa kituo uligharimu sh. milioni 94.677, ujenzi wa jengo la maabara (sh. milioni 52.440), ujenzi wa nyumba ya mtumishi (sh. milioni 36.299), ujenzi wa wodi ya wazazi (sh. milioni 106.303), ujenzi wa wodi ya watoto (sh. milioni 47.426) na ujenzi wa njia (Walk ways) kuunganisha majengo mapya (sh. milioni 36.805).

Pia, fedha hizo zilitumika kwa ajili ya ujenzi wa mfumo wa uvunaji, usambazaji na uhifadhi maji ambao uligharimu sh. milioni 26.118.

Anasema kazi ya ujenzi ilianza Julai 18, mwaka /2019 na kukamilika ndani ya miezi minne kama ilivyoelekezwa katika randama ya makubaliano ya kusimamia kazi ya ujenzi katika Halmashauri pamoja na mkataba baina ya fundi kiongozi na msimamizi mkuu wa ujenzi ambaye ni Mkurugenzi ...

Katika kipindi cha miaka mitano ya uongozi wa awamu ya tano, Halmashauri ya Wilaya Tandahimba imendeleza ujenzi wa zahanati 13 kwa vijiji vya Mnazimmoja, Mambamba, Miuta, Mitondi, Lembela, Malamba, Dinduma shuleni, Mkuti, Nachunyu, Chikongo, Milidu, Mtegu na Mitumbati. Uendelezaji wa Zahanati zote hizi umegharimu takriban sh. milioni 785 ambapo fedha zote hizo ni mapato ya ndani ya Halmashauri (Own source).

Aidha, Halmashauri imetumia sh. milioni 12, kutoka Mfuko wa Jimbo, kuendeleza ujenzi wa Zahanatihi na kufanya Jumla ya fedha zilizotumika kuendeleza ujenzi huo kufikia sh. milioni 797.

UKARABATI WA MAJENGO HOSPITALI YA WILAYA NA VITUO VYA AFYA

Katika kipindi cha miaka mitano halmashauri imefanya ukarabati wa majengo muhimu katika Hospitali ya Wilaya ya Tandahimba. Miongoni mwa majengo hayo ni pamoja na

kilichokuwa chumba cha kuhifadhi maiti Hospitali ya Wilaya, jengo la upasuaji, wodi ya kujifungulia, maabara na wodi ya wanaume (Grade) II.

UJENZI WA VITUO VYA AFYA

Halmashauri pia imechangia ujenzi wa vituo vya afya vitatu katika kata za Nanhyanga, Nambahu na Mdimba, ambao ulianzishwa kwa kutumia nguvu zawananchi. Fedha zilizotumika katika uendelezaji huo ni sh. milioni 23.920.

Akitoa mchanganuo wa fedha hizo, Msomoka anasema katika kuboresha Kituo cha Afya Nanhyanga, zilitumika sh. milioni 20 zilizotokana na mapato ya ndani ya halmashauri, Kituo cha Afya Mdimba, zilitumika sh. milioni 2.100, kutoka Mfuko wa Jimbo na Kituo cha Afya Nambahu nako zilitumika sh. milioni 1.820 pia kutoka mfuko huo na kufanya jmla kuu kuwa sh. milioni 23.

Anasema Halmashauri itaendelea kuchangia fedha katika vituo hivyo kadiri fedha zitakavyopatikana hasa mapato ya ndani. Pia, itaongeza mchango wake kwenye ujenzi wa zahanati pale ambapo wananchi wenyewe wataonyesha juhudi.

VIJANA, WANAWAKE WAMWAGIWA MIKOPO

Utoaji wa fedha za mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika kipindi cha 2015/2016-2019/2020 ilikuwa ni moja ya vipaumbele vya halmashauri.

Msomoka anasema Halmashauri ya Wilaya Tandahimba imeendelea kutoa mikopo kwa vikundi vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kulingana na sheria, kanuni na miongozo ya serikali ambapo, hadi kufikia mwaka wa fedha 2019/2020 jumla ya sh. milioni 893.954.

Mchanganuo wa fedha hizo ni kwamba sh. milioni 528.355, zilikuwa zimetolewa kwa vikundi 118 vya vijana, sh. milioni 335.945 zilitolewa kwa vikundi 77 vya wanawake n ash. milioni 29.654 kwa vikundi tisa vya watu wenye ulemavu.

KUHUSU ELIMU BILA MALIPO

Katika kipindi hicho Wilaya ya Tandahimba imepokea jumla ya sh. bilioni 2.687, kwa ajili ya kugharamia na kufanikisha mpango wa serikali wa

elimu bila malipo na fedha hizo zote zilitumika kwa kuzingatia mwongozo uliotolewa na serikali.

Aidha, anasema moja ya maeneo ambayo serikali ya awamu ya tano imeweka jitihada kubwa katika kipindi cha miaka mitano ni pamoja na ujenzi wa miundombinu mbalimbali katika shule za msingi kwa kutumia mapato ya ndani na fedha za ruzuku kutoka serikali kuu.

Kwa mujibu wa mkurugenzi, katika kipindi hicho halmashauri imeweza kujenga matundu 298 ya vyoonyo yenye thamani ya sh. milioni 193.752, pia imetekeleza ujenzi wa nyumba tisa za walimu zenye thamani ya sh. 122, hivyo kufanya jumla kuu kuwa sh. milioni 315.752 ambazo zote zinatokana na mapato ya ndani ya halmashauri.

Alisema pia Halmashauri ilipokea sh. milioni 554.707, kutoka serikali kuu kupitia program ya Lipa kulingana na Matokeo (EP4R). "Fedha hizi zilitolewa kwa mintarafu ya ukamilishaji na ujenzi wa vyumba vya madarasa shule za msingi."

Mkurugenzi alisema kati ya fedha hizo sh. milioni 100 zimetumika kujenga vyumba vitano vya madarasa, sh. milioni 11.899, zimekamiliha ujenzi wa matundu ya vyoonyo katika shule za msingi na sh. milioni 442.807, zimetumika kukamilisha vyumba vya madarasa 31 shule za msingi.

Pia, Kuanzia 2015/2016 hadi 2019/2020 halmashauri ilipokea sh. milioni 290, kutoka kwa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) ambazo zilitumika kwa kufuata miongozo ya serikali.

Kati ya fedha hizo sh. milioni 170, zimetumika katika ujenzi wa matundu 96 ya vyoonyo, na sh. milioni 120, zilitumika kujenga vyumba sita vya madarasa na ofisi kwa shule za msingi. Aidha, vyumba vyote vya madarasa na matundu hayo ya vyoonyo yamekamiliha na sasa yanatumika.

Vilevile katika kuhakikisha yanawekwa mazingira mazuri ya upatikanaji wa elimu bora, Juni 21, 2019, Wilaya ya Tandahimba kupitia Idara ya Uthibiti ubora wa shule, ilipokea sh. milioni 152.032, kutoka serikali kuu kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa ajili ya ujenzi wa ofisi ya Uthibiti Ubora wa Shule Wilaya.

Anasema kazi ya ujenzi ilianza Julai 18, mwaka /2019 na kukamilika ndani ya miezi minne kama ilivyoelekezwa katika randama ya makubaliano ya kusimamia kazi ya ujenzi katika Halmashauri pamoja na mkataba baina ya fundi kiongozi na msimamizi mkuu wa ujenzi ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba.

"Utaratibu uliotumika kutekeleza mradi huu wa ujenzi ni kutumia 'force akaunti' ambapo kamati tatu ambazo ni Kamati ya ujenzi, kamati ya manunuzi, na kamati ya mapokezi ziliundwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Tandahimba kwa ajili ya kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa mradi. Wajumbe wa



CHAGUA CCM



NYUMBA ya mwalimu shule ya msingi Mpunda

kamati hizo walitoka katika idara za Halmashauri, Uthibiti ubora wa shule na ofisi ya Mkuu wa Wilaya," alisema..

Aidha, Ofisihii ilitakiwa kuwa na maeneo muhimu yafuatayo; vyumba sita vya ofisi, ukumbi mdogo wa mikutano ya ndani ya idara, stoo, masijala, jiko na matundu manne ya vyoo vya jumua. Maeneo yote haya yamekamiliika na yanatumika.

Kwa mujibu wa mkurugenzi, halmashauri pia imefanikiwa kujenga kujenga ofisi mbili za tarafa na nyumba mbili za maofisa tarafa katika kata za Litehu na Mahuta zikiwa zimegharimu sh. milioni 185, ambapo Litehu ofisi na nyumba ya ofisa tarafa zimekamiliika na kuanza kutumika.

Kwa upande wa Mahuta ujenzi wa ofisi na nyumba uko katika hatua ya kuweka madirisha na milango, ambapo ofisi inagharimu sh. milioni 45 na nyumba sh. milioni 50.

KITUO CHA UFUNDI MATOGORO

Kituo cha ufundi Matogoro kipo katika shule mama ya msingi ya Matogoro. Kituo hiki kilianzishwa mwaka 2007 chini ya mwalimu Mkuu Hassani Chihako. Halmashauri imekifanyia ukarabati kituo hiki kwa gharama ya sh. milioni 30, kwa kutumia mapato ya ndani. Halmashauri pia imetoa sh. milioni 40.480, kwa lengo la kununua vifaa vinavyohitajika kwa mafunzo ya kila siku, na kufanya jumla ya fedha zilizotolewa na halmashauri kwa chuo hiki kufikia sh. milioni 70.480.

Mbali na hilo, alisema mwaka 2018 Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba ilipokea msaada kutoka Shirika lisilokuwa la Kiserikali la Eclat Development Foundation (ECLAT).

"Msaada huu haukuwa fedha tasilimu bali ni ukarabati wa vyumba vya madarasa vinane, ujenzi wa matundu 32 ya vyoo na ukarabati wa kisima cha kuvuna maji ya mvua chenye uwezo wa kuhifadhi lita 100,000. Shughuli zote hizi zimefanyika Shule ya Msingi Luagala "A". Gharama za ukarabati na ujenzi wa miundombinu yote Shule ya Msingi Luagala "A" ni sh. Milioni 131.500," alisema.

Anasema mwaka 2019 shirika hilo la Eclat Development Foundation lilitoa msaada wa ujenzi na ukarabati wa madarasa, kuchimba kisima cha maji na kujenga matundu ya vyoo katika Shule ya Msingi Luagala B.

Majengo yaliyokarabatiwa ni vyumba sita vya madarasa, ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa ununuzi wa meza 16 na viti 16, matundu 16 ya vyoo na ukarabati wa kisima cha kuvuna maji ya mvua.

"Gharama za ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya shule ya msingi Luagala "B" ni sh. milioni 142.133. Jumla ya gharama ya miradi yote miwili, Shule ya Msingi Luagala "A" na Shule ya Msingi Luagala "B" ni sh. milioni 273.633," alisema.

Barabara za lami zaongezeka, walimu wapata makazi bora

MAKAZI BORA KWA WALIMU

Mwaka 2017 Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba ilipokea sh. milioni 150, kutoka serikali kuu kupitia mradi wa Lipa kulingana na Matokeo (EP4R). Fedha hizi zilitolewa kwa mintarafu ya ujenzi wa nyumba sita za walimu shule ya Sekondari Tandahimba. Fedha hizi zilitolewa na serikali kutokana na wananfunzi wa kidato cha sita kufaulu mitihani kwa asilimia 100. Kazi ya ujenzi ilikamilika 2017 na nyumba zinatumiwa.

Aidha, katika kipindi cha 2015/2016 hadi 2019/2020 Halmashauri ya Tandahimba ili kukabiliana na changamoto ya upungufu wa vyumba vya madarasa na samani, ilifanikiwa kujenga vyumba 52 kwa shule za sekondari vyenye thamani ya sh. milioni 834.200. Pia, ilitengeneza madawati 8,565 yenye thamani ya sh. milioni 877.800, kwa shule za msingi na Sekondari.

Vilevile Halmashauri ilipokea sh. milioni 150, kwa ajili ya ujenzi wa vyumba sita vya madarasa shule za sekondari. Fedha zote zimetumika kujenga nyumba sita za walimu katika Shule ya Sekondari Tandahimba

iliyopo Tandahimba mjini, ambazo zimilika na sasa zinatumiwa.

Pia, Halmashauri ya Tandahimba imetumia sh. milioni 336 kutoka katika mapato yake ya ndani, kuweka mfumo wa maji safi na maji taka katika vyumba vya maabara 69 kwa shule za Sekondari. Lengo la mpango huo ni kuhakikisha maabara zinatumiwa na wananfunzi kama ilivyokusudi.

"Halmashauri itaendelea kutenga fedha ili kukamilisha vyumba vyote 77 vya maabara ili navyo vitumiwe na walimu na wanafunzi kwa ajili ya kujifunzia na kufundishia masomo ya sayansi," alisema.

BARABARA ZALAMI

Wilaya ya Tandahimba katika kipindi hiki cha miaka mitano imefanikiwa kujenga kilomita tatu za barabara kwa kiwango cha lami katika eneo la Tandahimba mjini. Barabara hii imejengwa kwa kutumia mapato ya ndani ya Halmashauri. Ujenzi wa barabara hii umegharimu jumla ya sh. bilioni 1.38 zilizotokana na mapato ya ndani ya halmashauri (Own source), sehemu kubwa ya mapato hayo yametokana na ushuru wa zao la korosho.

Pia, Serikali iliamua kujenga barabara kwa kiwango cha lami kipande cha kilomita 2.4 katika eneo la Namikupa katika barabara ya Namikupa-Maundo. Barabara hii imejengwa kwa gharama ya sh. bilioni 1.976. Fedha hizo ni kutoka Mfuko wa Barabara. Barabara hii imejengwa na Mkandarasi Chibeshi Construction Limited Kampuni ya wazalendo wa Mkoa wa Mtwara.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, barabara hiyo imejengwa kwa awamu mbili; awamu ya kwanza ilijengwa kilomita 1.2 na awamu ya pili nayo ilikuwa na kilomita 1.2 na kufanya jumla ya kipande chote kuwa kilomita 2.4.

"Ujenzi wa barabara hii umeleta faraja kubwa kwa wananchi wa Wilaya ya Tandahimba, kwani mteremko huu (Namikupa) umeleta hasara kubwa kwa watu binafsi pia



Moja kikundi cha ufundi seremala ambacho kimefaidika na mikopo ya vijana



BARABARA ya Namikupa kwenda maundo



CHAGUA CCM

Zahanati zaongezeka, huduma za afya zaboreshwa



ZAHANATI ya Mtegu

hata upande wa serikali. Kabla ya kujengwa kwa kiwango cha lami magari yaliyokuwa yakisomba korosho toka vijijini, yalikuwa yanaanguka kisha kusababisha hasara ya mamiloni kwa kupoteza korosho zilizokuwa zijipelekwa kwenye maghala ya Chama Kikuu cha Ushirika (TANECU), Newala, Tandahimba hadi Mtwara.

Pia, ajali zilizokuwa zikitokea katika eneo hilo zimesababisha kupoteza maisha ya watu na wengine kupata ulemavu wa kudumu. Wafanyabiashara wamepoteza mali zao nyingi zenye thamani ya mamiloni ya fedha.

"Hivyo wananchi wanaishukuru serikali inayoongozwa na Rais Dk. John Magufuli kwa kuwaondolea adha mbalimbali zilizotokana na kipande hiki ambacho sasa kimejengwa kwa kiwango cha lami. Tunamuomba Rais atusaidie tena kujenga kwa kiwango cha lami eneo la Sinyangi, barabara toka Tandahimba kwenda Mchichira kwani nayo ni barabara muhimu kwa usafiri na usafirishaji kwa wakazi wa wilaya ya Tandahimba na nchi jirani ya Msumbiji," alisema.

MAJI YAWAFIKIA WANANCHI

Mradi wa maji Mkwiti umeanza rasmi utekelezaji Januari 30, 2018 na umefikia katika hatua nzuri.

Mpaka kukamilika unakadiriwa kutumia sh. bilioni 8.5 kwa fedha za mfuko wa maji. Kutokana na ufyni wa bajeti utekelezaji wa mradi umegawanywa katika awamu nne Awamu ya kwanza unafanywa na Mkandarasi Mshamindi Costruction LTD & EDGEPOINT Co.LTD kwa gharama ya sh. bilioni 3.271.

Kazi zilizopangwa kufanyika katika awamu hii ni ujenzi wa bomba kuu la maji kutoka chanzo cha maji Mitema - Kitangali kilichopo Wilayani Newala hadi kijiji cha Idamnole kwa umbali wa kilomita 13.9 na ujenzi wa

tenki la kuhifadhi maji juu ya ardhi lenye lita 500,000 katika Kijiji cha Idamnole. Utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 70. Kazi zilizofanyika ni ujenzi wa bomba kilomita tisa na msingi wa tenki.

Hata hivyo, Aprili 19, 2020 mkataba ulivunjwa kutokana na mkandarasi kushindwa kukamilisha kazi kwa wakati. Kutokana na kuvunjwa kwa mkataba ofisi ya Meneja Wilaya iliomba kibali cha kuendelea na utekelezaji kutoka wizara ya maji ambacho kilishatolewa na mradi huu kwa sasa utajengwa kwa kutumia watalaamu wa ndani (force account). Kwa sasa taratibu za ununuzi zinaendelea ili kuendelea na utekelezaji.

Awamu ya pili inatekelezwa na Mamlaka ya Maji Mtwara (MTUWASA) kwa kutumia watalaamu wa ndani (force account) kwa gharama ya sh. bilioni 1.890, na sh. milioni 570, zilishatolewa. Kazi zilizopangwa kufanyika ni ujenzi wa bomba kilomita 17.1 kutoka Kijiji cha Idamnole hadi Kijiji cha Mangombya, na tenki la lita 300,000, juu ya ardhi katika Kijiji cha Mangombya.

Utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 83, na kazi zilizofanyika ni ujenzi wa bomba kilomita 16.1 na ujenzi wa tenki. Utekelezaji wa mradi awamu ya tatu na ya nne utaanza baada ya kibali cha kuendelea kutolewa na Wizara ya Maji.

"Mradi huu utakapokamilika tunatarajia utanufaisha jumla ya watu 21,384 katika vijijij 15 vya

Wilaya ya Tandahimba ambavyo ni Mangombya, Nanjanga, Mkwitijuu, Mkwiti chini, Ngunja, Nannala, Chidede, Namindondijuu, Namindondichini, Mabeti, Mmeda, Litehu, Libobe, Mkolajuu na Mkuti pamoja na vijiji viwili vya Mahoha na Nam-bali vilivyopo wilaya ya Newala ambavyo vinapitiwa na mradi," alisema.

CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA

Moja ya changamoto zilizojitokeza katika kipindi hicho ni pamoja na uhaba wa mafundi ujenzi (uashi na useremala) waliosomea na wenye uwezo wa kusoma na kutafsiri ramani mbalimbali za majengo na vifaa vingine. Hatua hii inachangia kuchelewesha kazi kwani inamlazima Mhandisi wa Ujenzi kutumia muda mwingi kutoa maelekezo, hata hivyo baadhi yao wanashindwa kufuata maelekezo hatimae kusababisha hasara kwa halmashauri.

Uhaba wa maji, sehemu kubwa ya Wilaya ya Tandahimba ni kame hasa wakati wa kiangazi, hivyo baadhi ya miradi ya ujenzi inachelewa kukamilika, pia kutofikia ubora wake kutokana na ukosefu wa maji wa kutosha kujengea na kumwagilia. Mfano matofali na zege.

Kuchelewa kuingiziwa fedha au kuingia fedha nje ya Bajeti ambapo hulazimika kutumia muda mwingi kuzitafutia vifungu kwenye mfumo wa Bajeti (PlanRep). Uchakavu wa baadhi ya

barabara katika maeneo ya Vijijini husababisha upelekaji wa vifaa vya ujenzi kuwa mgumu; mfano barabara za Lipalwe, Chikumbillo na Chiumo. Mara nyingi miradi inapotekelezwa katika maeneo haya hutumia muda mrefu kutokana na uchakavu wa barabara hatimae usafirishaji wa vifaa vya ujenzi kwenda maeneo hayo huwa ni shida na ni gharama kubwa kuliko menea mengine.

WANANCHI WAJIVUNIA

Zubeir Nyambombwe mkazi wa Tandahimba mjini, alisema miaka mitano ya Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Rais Magufuli imemtoa katika ngazi ya chini ya makazi ambapo sasa amejenga nyumba bora.

"Nashukuru na kujivunia hilo kwa kweli. Nilikuwa sina nyumba bora lakini sasa ninaishi katika nyumba ya kisasa, watoto wangu wanakwenda shule na kurudi katika mazingira mazuri kabisa," alisema.

Alisema mafanikio aliyopitia yana msaada mkubwa na juhudi zilizofanywa na serikali katika kuboresha hali za wakulima na wananchi kwa ujumla.

Kwa upande wake, Juliana Kindole mkazi wa Kijiji cha Chidede, alisema jambo kubwa analoweza kuipongeza serikali ni kufikisha maji karibu na makazi ya watu. "Hii ilikuwa changamoto kubwa kwetu hasa kinamama, tunamshukuru Rais Magufuli na wasaidizi wake walioko huku wilayani kwa kweli wanafanya kazi nzuri."

"Nashukuru na kujivunia hilo kwa kweli. Nilikuwa sina nyumba bora lakini sasa ninaishi katika nyumba ya kisasa, watoto wangu wanakwenda shule na kurudi katika mazingira mazuri kabisa," alisema.



WANAFUNZI wa Shule ya sekondari Nachunyu, wakiwa darasani.